035713655

KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS

# KCPE

516004

# KISWAHILI
# SEHEMU YA KWANZA
# LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

**NAMBA YAKO YA MTIHANI**
**JINA LAKO**
**JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
A. waraka
B. barua maalum
C. barua ya kiofisi
D. Barua rasmi

Jibu sahihi ni **D**

**Katika karatasi ya majibu:**

**2.** [A] [B] [C] [D] **12.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D] **42.** [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© Mtihani Bora

**GEUZA UKURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Nchi ya Kenya ___1___ kama ___2___ mataifa mengine, huwa'na makundi ya watu wenye ___3___ mbalimbali. Kila mojawapo ya ___4___, huwa na lugha yake mahsusi ambayo ___5___ wanajamii wote. ___6___ baadhi ya makundi ni makubwa ___7___ mengine, ni muhimu kuelewa kwamba lugha zote ni sawa. Mwanajamii ___8___ ___9___ kuionea lugha yake na kujitahidi kuizungumza.

1. A. ,  B. ;  C. __  D. :
2. A. ilivyo  B. yaliyo  C. kulivyo  D. yalivyo
3. A. utangulizi  B. chimbuko  C. asiria  D. mwenendo
4. A. kundi hili  B. kundi hizi  C. makundi hawa  D. makundi haya
5. A. huwahifadhi na kuwatuza  B. huwaidhinisha na kuwatukuza  C. huwatambulisha na kuwaunganisha  D. huwaelekeza na kuwawasilisha
6. A. Japo  B. Lau  C. Ilhali  D. Kwani
7. A. kuyaliko  B. kuziliko  C. kuliko  D. kuwaliko
8. A. yoyote  B. yeyote  C. wowote  D. kokote
9. A. hana budi  B. ana budi  C. huna budi  D. hamna budi

___10___ la mahakimu ___11___ kesi ile kwa makini. Wakili wa mshtakiwa alijitahidi kumtetea mteja wake aliyesimama pale ___12___. Hata hivyo, ushahidi ___13___ ulidhihirisha waziwazi kwamba mshtakiwa alikuwa na hatia. Kwa hakika ___14___. Mara hii ___15___ kuruka kesi kama alivyozoea kufanya hapo awali alipokabiliwa na mashtaka.

10. A. Genge  B. Jeshi  C. Furushi  D. Jopo
11. A. walisikiliza  B. ilisikilizwa  C. walisikiliza  D. lilisikiliza
12. A. jukwaani  B. kizimbani  C. faraghani  D. ulingoni
13. A. uliotolewa  B. iliyotolewa  C. uliyotolewa  D. iliyotolewa
14. A. Hasidi mpe kiti akae  B. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu  C. Mbio za sakafuni huishia ukingoni  D. Akimbiaye huagana na nyonga
15. A. akaweza  B. hakuweza  C. hawezi  D. akiweza

***<u>Kutoka swali la 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.</u>***

16. **Bainisha matumizi ya kiambishi ka kwenye sentensi ifuatayo.**
Saumu ameenda hospitalini akatibiwe.
    A. Kuonyesha kuendelea kwa jambo.
    B. Kuonyesha kufuatana kwa matukio.
    C. Kuonyesha wakati uliopita.
    D. Kuonyesha kusudi la jambo.

17. **Chagua wingi wa sentensi ifuatayo.**
Mtume alisimama karibu na ua wa nyumba hiyo.
    A. Mitume walisimama karibu na nyua za nyumba hizo.
    B. Watume walisimama karibu na maua ya nyumba hizo.
    C. Mitume ilisimama karibu na maua ya nyumba hizo.
    D. Watume walisimama karibu na nyua za nyumba hizo.

18. **Ainisha maneno yaliyoangaziwa katika sentensi ifuatayo.**
Tunda hilo <u>bivu</u> ni lako lakini <u>lile</u> jingine litawekwa <u>kikapuni</u>.
    A. kiwakilishi, kiwakilishi, nomino
    B. kivumishi, kivumishi, kielezi
    C. kivumishi, kiwakilishi, kielezi
    D. kiwakilishi, kivumishi, nomino.

19. Neno '<u>mchafuzi</u>' lina sauti ngapi?
    A. 4
    B. 7
    C. 8
    D. 3

20. **Kanusha sentensi ifuatayo.**
Musa anazifua nguo akizianika kwenye kamba.
    A. Musa hajafua nguo wala kuzianika kwenye kamba.
    B. Musa hafui nguo akizianika kwenye kamba.
    C. Musa hakufua nguo akizianika kwenye kamba.
    D. Musa hafui nguo kwa kuzianika kwenye kamba.

21. Chagua maelezo yaliyo sahihi.
    A. Pwaga ni kuchemka kwa chakula lakini bwaga ni kuangusha kitu kwa nguvu.
    B. Janja ni kuwa mwerevu lakini chanja ni kuunganisha kitu kilichopasuliwa.
    C. Kogo ni sehemu ya nyuma ya shingo lakini gogo ni kipande cha mti uliokatwa.
    D. Shua ni kuteremsha chombo lakini sua ni kutia maji kinywani ili kukisafisha.

22. Chagua viambishi kwenye neno <u>chekana</u>.
    A. che-an-a
    B. chek-an-a
    C. a -na
    D. an-a

23. Mfuko wa ngozi ambao hutumiwa na wahunzi kupulizia moto ni
    A. tishali
    B. jiriwa
    C. mvukuto
    D. huka.

24. **Andika sentensi ifuatayo katika kauli ya kutendea.**
Masi aliyachota maji ya bibi.
    A. Bibi alichotewa maji na Masi.
    B. Masi alichotea maji kwa bibi.
    C. Masi alimchotea bibi maji.
    D. Maji yalichotwa na Masi kwa bibi.

25. Ombi la kutaka kesi isikilizwe upya baada ya hukumu ya kwanza kutolewa ni
    A. kukata notisi
    B. kukata rufaa
    C. kuahirisha kesi
    D. kutoa dhamana.

26. Bainisha maelezo yaliyo sahihi.
    A. Mlowezi ni mtu anayeipenda sana nchi yake.
    B. Mhaini ni mtu aliyehamia nchi nyingine na kumiliki ardhi huko.
    C. Mkiritimba huwazuia wengine kufanya biashara ili afaidike.
    D. Kibaraka huitawala nchi yake kwa mabavu.

27. Kivumishi kinachoweza kuundwa kutokana na kitenzi 'nyamaza' ni
    A. nyamavu
    B. kunyamaza
    C. unyamavu
    D. nyamaa.

28. **Tegua kitendawili kifuatacho.**
Mke wangu mfupi lakini huvaa nguo nyingi.
    A. Hindi
    B. Kope
    C. Nyuki
    D. Ndizi.

29. **Tambua fani za lugha zilizotumika katika sentensi hii.**
Siku hiyo nilikuwa kunguru, moyo wangu ukaniambia nichane mbuga.
    A. tanakali, chuku, nahau
    B. sitiari, tashhisi, nahau
    C. tashhisi, kinaya, tasfida
    D. sitiari, chuku, nahau.

30. **Ni methali gani inayoambatana vyema na maelezo haya?**
Hata jambo liwe gumu vipi, panapo bidii na subira, lazima litatimizwa.
    A. Ada ya mja hunena mwungwana ni kitendo.
    B. Mchumia juani hulia kivulini.
    C. Maji ukiyavulia nguo huna budi kuyaoga.
    D. Abadi abadi kamba hukata jiwe.

Geuza ukurasa

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 31 mpaka 40.**

Katika siku za hivi karibuni, suala la kuongezeka kwa visa vya maradhi yasiyo ya kuambukiza limewatia washikadau wa sekta ya afya kiwewe. Kati ya maradhi yaliyoenea vururu ni shinikizo la damu, kisukari na aina mbalimbali za saratani. Awali, visa hivi vilihusishwa sana na watu wenye kipato kikubwa na wale wenye umri wa juu. Hata hivyo, hali imebadilika sasa ambapo visa hivi vinaripotiwa sana hata miongoni mwa vijana na watoto.

Je, ni mambo yapi yanayochangia zaidi katika hali? Uhamiaji wa watu kutoka sehemu za mashambani hadi mijini umewafanya wengi kubadili hali yao ya maisha. Mathalani, watu ambao hapo awali walikuwa wakipiga milundi kuelekea kwenye shughuli zao huanza kuabiri vyombo vya uchukuzi hata wanaposafiri masafa mafupi. Kule kazini wanatumia mitambo kupanda kwenye majengo. Ofisini nako wanashinda kwenye tarakilishi kutwa nzima. Siha yao nayo huanza kudhoofika polepole.

Si suala la mjadala kuwa watu wameyasusia maakuli ya kiasili kama vile mihogo, viazi vitamu, mboga za kinyeji na matunda. Badala yake wanabugia vyakula kama vibanzi, kuku wa kubanika, keki, mikate na soda. Vingine ni vyakula vinavyoandaliwa viwandani ambavyo aghalabu huwa vimesheheni kemikali za kila aina. Watu hawa wamo katika hatari ya kuugua kisukari, shinikizo la damu na maradhi ya moyo kwa kunenepa kupita kiasi.

Burudani ni sababu nyingine inayochangia kuongezeka kwa visa hivi. Ukitupa macho katika maeneo ya starehe, hukosi kuwaona adinasi wanaobugia vileo vya kila aina. Uraibu wa pombe umehusishwa sana na maradhi ya ini na figo. Watu wenye shinikizo la damu wakizoea kubugia vileo huzorotesha hali zao; jambo ambalo linaweza kuwafanya **<u>watuache mkono</u>**. Uvutaji wa sigara umehusishwa sana na saratani ya mapafu na ile ya mdomo. Hatuna budi kuzingatia uraibu unaofaa, vinginevyo tutajipata katika msiba wa kujitakia ambao hauna kilio.

Uchochole ni sababu kuu inayolemaza juhudi za wengi za kudumisha rai zao. Watu wengi hawawezi kumudu gharama ya lishe bora kutokana na kuongezeka kwa bei hasa ya mboga na matunda. Isitoshe, ni vigumu kwa mahuluku hawa kupata nyenzo za kufanyia mazoezi. Hata hivyo, hiyo siyo sababu tosha kwani si lazima mtu awe na nyenzo mbalimbali ili ashiriki mazoezi ya viungo. Husemekana kuwa, **<u>ukikosa la mama hata la mbwa huamwa</u>**.

Mti hauendi ila kwa nyenzo. Kuimarika kwa afya ya mtu hakutamjia vivi hivi tu bali kila mmoja anahitajika kujibidiisha siha yake kwa kuandama mienendo ifaayo. Walio katika hatari kubwa zaidi ya kuugua maradhi yasiyo ya kuambukiza ni wale walio na umri mkubwa, wanaotoka katika familia zenye visa vya magonjwa haya, watumiaji wa vileo na wenye unene uliopita kiasi. Watu hawa wanashauriwa kufanyiwa uchunguzi mara kwa mara, kufanya mazoezi na kula vizuri ili kupunguza hatari hii. Halikadhalika, hatuna budi kuzingatia usafi wa mazingira ili kuwinga hatari hii.

Serikali aidha ina wajibu wa kutekeleza. Kwanza ni kushirikiana na vyombo vya habari pamoja na mashirika yasiyo ya kiserikali kuelimisha umma jinsi ya kujiepusha na maradhi haya. Pili, huduma za afya zinapaswa kuimarishwa ili kuwezesha kuchunguza na kudhibiti maradhi haya miongoni mwa wananchi. Bidhaa za kimsingi nazo zipunguzwe bei ili kuondoa mzigo wa lishe bora. Aidha, ni muhimu kuwekeza katika utafiti utakaofanikisha uvumbuzi wa tiba ya magonjwa haya kwani penye nia pana njia.

31. Kulingana na aya ya kwanza, ni kweli kuwa
A. idadi ya watu inayoambukizwa maradhi imeongezeka sana siku hizi
B. kudhoofika kwa watu wengi kiafya kumewatia wasiwasi wahusika wa sekta hiyo
C. uele uliozagaa zaidi miongoni mwa wanajamii ni shinikizo la damu
D. magonjwa mengi wanayougua watu yanatokana na ulaji wa sukari.

32. Tofauti iliyopo baina ya nyakati hizi na zile za zamani kulingana na kifungu ni kuwa
A. kinyume na awali wanaougua sana sasa ni watu wenye uwezo wa kifedha
B. kando na ilivyo sasa, awali vijana na watu wasio na kipato kikubwa ndio walioathirika zaidi
C. kinyume na awali, magonjwa yaliyopo sasa hayawezi kidhibitiwa.
D. kando na hapo awali, wanaougua sasa ni wa kila tabaka na umri.

33. Kulingana na aya ya pili, ni kweli kusema kuwa
A. uhamiaji wa watu mijini umewasababishia kudhoofika kiafya
B. ukosefu wa mazoezi ya viungo unaweza kumfanya mtu aathirike kiafya
C. kutumia vyombo vya uchukuzi kumeongeza visa vya maradhi
D. wanaotumia tarakilishi wamo katika hatari kubwa zaidi.

34. Vyakula vya kiasili
A. vinachangia kuepuka baadhi ya maradhi
B. si vizuri kama vile vinavyotengenezwa viwandani
C viliwafanya watu wengi kukonda na kukondeana
D. havikuliwa na watu wenye hatari ya maradhi.

35. Hali anayopinga mwandishi katika aya ya nne ni
A. matumizi mabaya ya vileo
B. tabia ya watu wanaoshiriki burudani
C. kuongezeka kwa maradhi ya ini na figo
D. watu wenye saratani ambao wanavuta sigara.

36. Sababu kuu inayowafanya watu kuathirika kiafya kulingana na makala haya ni
A. shughuli za kikazi
B. uharibifu wa mazingira
C. ukosefu wa rasilimali
D. kukosa elimu.

37. Methali '<u>**ukikosa la mama hata la mbwa huamwa**</u>' jinsi ilivyotumika ina maana kwamba
A. si lazima mtu awe tajiri ili ale mboga na matunda
B. umaskini hauwezi kumzuia mtu kupata nyenzo atakazo
C. kukosa lishe bora si sababu ya kutofanya mazoezi
D. mtu anaweza kuvinyoosha viungo hata pasipo na nyenzo mahsusi.

38. Msimamo wa mwandishi wa makala haya ni kuwa
A. ukitaka kuimarika kiafya lazima uwe na kila kitu kinachofaa
B. kuugua mara kwa mara ni ishara ya mazoea mabaya
C. ni vigumu mtu kuwa na afya ikiwa familia yake imeathirika
D. ili mwili uwe na nguvu sharti mtu awajibike katika kuutunza.

39. Kulinga na aya ya mwisho, yote haya yatachangia kuwepo jamii yenye afya asipokuwa
A. kuelimisha umma kuhusu mienendo ifaayo
B. kufanya utafiti kuhusu magonjwa yaliyotajwa
C. kuelimisha mashirika yasiyo ya kiserikali kuhusu uwajibikaji
D. kuwapunguzia wananchi gharama ya bidhaa

40. Msemo '<u>**watuache mkono**</u>' una maana sawa na
A. wafe moyo
B. mkono wa tanzia
C. watangulie mbele ya haki
D. waende nguu

**Geuza ukurasa**

**_Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu swali la 41 mpaka 50._**

Katika kitongoji kimoja, aliishi mzee aliyeitwa Bwana Hekima. Wanakijiji walimwenzi mzee huyu kwa mengi. Alikuwa mzee mpole mwenye mkono wazi. Hakika, wote waliotangamana na mzee huyu, walielewa waziwazi maana ya methali kutoa ni moyo usambe ni utajiri. Ungemweleza shida yako, ungemwona amekutumbulia macho kwa makini huku akitikisa kichwa kuitikia. Hatimaye, angekufaa kwa chochote alichokuwa nacho au akuelekeze utakakosaidika. Wakati mwingine hata alikopa kwingine almradi awafae wahitaji.

Mzee huyu alijaliwa wana wawili wa kiume. Alijaribu kuwalea kwa misingi ya maadili kwani aliamini kuwa mtu hujengwa na utu bali si kitu. Siku zote aliwahimiza umuhimu wa kuungana na majirani kwani mtu pweke ni uvundo. Vijana walimwiga baba yao kwa mengi tangu kuinamia cha mvunguni, kuwahurumia wasiobahatika katika jamii na hata kutumia lugha ya heshima. Hata hivyo kama walivyosema wahenga hakuna kizuri kikosacho ila. Kadri vijana hawa walivyoendelea kukomaa, ndivyo moyo wa ushindani ulivyozidi kutia doa uhusiano wao. Hakika walikuwa **hawapikiki katika chungu kimoja**.

Kijana mdogo alijiamini sana kwani biashara yake ilivuta kimo zaidi. Hakika, aliianzisha biashara hii katika muda mfupi kisha ikastawi kama mgomba. Kwa njia hiyo, alimwona nduguye mkubwa aliyejihusisha na kilimo cha mimea na ufugaji kama aliyekosea dira ya maisha. Kila alipopata nafasi ya kumkejeli mbele ya watu hakukosa kukinaishi hamu hiyo. Baba yake alimwonya si mara moja, si mbili. Akamkumbusha kuwa mpanda ngazi hushuka. Hata hivyo, kijana huyu alikuwa ameyatia masikio yake komango na tangu hapo jitihada zote za kumnasihi ziligonga ukuta. Kwa upande wake, kijana mkubwa aliamini kuwa licha ya masimango ya ndugu, uhusiano wao wa damu ulikuwa muhimu zaidi.

Wakati mmoja, ulianzishwa mradi wa watu kuwekeza kiasi kidogo cha fedha katika shirika fulani lililolipa riba ya juu baada ya muda mfupi. Kijana mdogo **aliiona hii kama njia bora zaidi ya kufurisha kibindo chake.** Kwa mara ya kwanza aliwekeza kiasi kidogo kwa tahadhari. Hayakupita hata majuma mawili, akajipatia kipato kikubwa maradufu akilinganisha na fulusi alizowekeza. Mara hii aliamua kutumia pesa nyingi kuliko zile za awali. Mradi huu ulikuwa umepata umaarufu mkubwa sasa. Wote waliowekeza sasa hawakuwa na wasiwasi wowote nao walitimiziwa haki yao kama walivyoahidiwa.

Mwishowe, kijana aliamua kupiga bei mali yake yote, akiwa na uhakika wa kuchuma zaidi. Hapo alijiona akijijengea kasri kubwa viungani mwa mji, aondokee 'bughudha' za kakaye kijijini. Alijiona akiwa amenunua shangingi kubwa ambalo lingemsaidia kukabiliana na barabara mbovu za kijiji kwani bado alipanga kufika kule mara mojamoja kumjulia hali babaye. Laiti angalijua!

Siku ya kupokea mapato ilifika. Kijana na wawekezaji wenzake wakawa na matumaini makuu. Hata hivyo, nusura wazirai walipofika ofisini. Ofisi zote zilikuwa zimefungwa. Juhudi za kuwasiliana na wakuu wa shirika na makarani wao ziliambulia kidole gutu. Kijana na wenzake hawakutaka kuukubali ukweli uliokuwa bayana kwao. Walikuwa wametapeliwa. Wanahabari ndio waliojaribu kuwaliwaza huku wakiwahoji kuhusiana na yale yaliyojiri. Laiti wangalijua kuwa mwisho wa tamaa ni tama na yote yang'aayo si dhahabu. Kijana aliona vimulimuli ghafla akaghumiwa.

Ndugu mkubwa alipokea habari zile kupitia kiredio alichokuwa nacho shambani. Hapo alitieleka jembe lake, akajiandaa himahima kuenda kumuaini mnuna wake. Hakika damu ni nzito kuliko maji.

41. Chagua jibu lililo sahihi kulingana na kifungu hiki.

A. Mzee alikuwa na sifa ya kutotangamana na watu.

B. Watu walijifunza ukarimu kutokana na hulka ya mzee.

C. Mzee anayezungumziwa alikuwa tajiri mkubwa.

D. Watu walishangaa waliposaidiwa na mtu maskini.

42. Mzee alipomtumbulia macho mzungumzaji

A. ni ishara kwamba alikuwa msikilizaji bora

B. alikuwa ameshangazwa na mzungumzaji

C. alinuia kumkatalia ombi lake mzungumzaji

D. inaonyesha kwamba hakumsikia mnenaji vizuri.

43. Vijana walijifunza sifa zifuatazo kutoka kwa baba yao ila

A. unyenyekevu

B. ukarimu

C. bidii

D. udugu.

44. Msemo **'hawapikiki katika chungu kimoja'** unaonyesha kuwa ndugu hawa

A. hawakuishi pamoja

B. hawakutengana

C. hawakupatana

D. hawakuhusiana kiukoo.

45. Kijana mdogo alipenda kumkejeli mkubwa wake kwa kuwa

A. alimwonea gere kwa mafanikio yake

B. biashara ya ndugu mkubwa iliendelea vizuri

C. alijiona kuwa bora kuliko kaka yake

D. kijana mdogo alikuwa mwenye akili zaidi.

46. Si kweli kusema kuwa

A. kijana mkubwa alitamani mdogo wake aharibikiwe na mambo maishani

B. kijana mdogo alipewa ushauri ila hakuuzingatia

C. kijana mkubwa alijali maslahi ya mnuna wake

D. kijana mdogo alijaliwa ufanisi zaidi ya mkubwa wake.

47. "**Aliiona hii kama njia bora zaidi ya kufurisha kibindo chake**" ndiko kusema

A. aliamua kutumia udanganyifu ili atajirike zaidi

B. alivutiwa na njia ile kwa kuamini kuwa ingemwimarisha zaidi kiuchumi

C. aliiona ile kuwa njia bora zaidi ya kutumia akiba yake

D. aliamini kuwa ile ni njia bora zaidi ya kuonyesha ujanja wake.

48. Ni dhahiri kwamba walioanzisha mradi husika walikuwa

A. majambazi

B. wachopozi

C. walowezi

D. matapeli.

49. Kwa nini wawekezaji walipata ofisi zimefungwa?

A. Wahalifu walitoweka baada ya kutimiza uovu wao.

B. Kuongezeka kwa wateja kulisababisha ofisi ihamishwe.

C. Wawekezaji hawakufika kwa wakati uliohitajika.

D. Wahalifu walikuwa wametiwa mbaroni na polisi.

50. Funzo linalojitokeza katika kifungu hiki ni kuwa

A. Tusiwategemee marafiki kwani hawawezi kutusaidia kama ndugu wakati wa dhiki.

B. Tujitenge na watu wanaotudhalilisha kwani hawana shukrani maishani.

C. Tusivutiwe na mambo yaonekanayo mazuri bila kuyachunguza vizuri ili tusije kuhasirika

D. Tutumie maarifa tuliyojaliwa kujifaidi ipasavyo maishani.

**Geuza ukurasa**

**Andika Insha ya kusisimua juu ya:**

**Kulima mavune, kuvuna vicheko**